Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

*HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA*

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# MUHTASARI

*Muhtasari huu ni dondoo muhimu zilizochambuliwa kutoka katika kila kitini kumwezesha msomaji apate uelewa wa haraka kuhusiana na masuala muhimu ndani ya Idara ya Wanyamapori. Wakati muhtasari huu ukitoa habari kwa ufupi, inapendekezwa kuwa kila kitini cha kisera kisomwe chote ili kupata uelewa mzuri wa masuala muhimu katika sekta ya wanyamapori kupitia takwimu na ushaidi uliotolewa.*

## CHAPISHO NA. 1: MWISHO WA WANYAMAPORI? KUPUNGUA NA KUHARIBIWA KWA WANYAMAPORI TANZANIA

MASUALA MUHIMU:

⇨ Takwimu bora na za kisasa zinapendekeza kuwa wanyamapori wanapungua katika maeneo yote muhimu ya wanyamapori na mifumo ya uhifadhi Tanzania, ikiwa ni pamoja na maeneo makubwa yaliyohifadhiwa kama vile Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba.

### Tanzania ina maeneo makubwa na wanyama wengi duniani

Tanzania ina idadi kubwa ya wanyama wakubwa waliobaki kupita taifa lolote lile duniani. Tanzania ndiyo yenye idadi kubwa kabisa ya simba na nyati wengi zaidi. Na idadi ya tembo inayoongezeka inakaribia na ile ya Botswana ambayo ina idadi kubwa Barani Afrika. Makundi ya wanyamapori katika mifumo ya ikolojia ya Serengeti – zaidi ya pundamilia milioni mbili, nyumbu, jamii ya swala – ya mkini inawakilisha mkusanyiko mkubwa wa wanyamapori waliobaki katika sayari yetu. Tanzania imeanzisha moja ya mitandao mikubwa ya maeneo yaliyohifadhiwa kuliko nchi yoyote ile duniani, takribani asilimia 30 ya eneo la nchi limehifadhiwa kama Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi.

Idadi ya wanyamapori Tanzania imetawanyika wakipatikana ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa mahali ambako wanaishi na binadamu katika ardhi za vijiji na za watu binafsi. Wanyamapori ni msingi wa biashara ya utalii wa kupiga picha na ya uwindaji na hivyo, ni raslimali muhimu ya kiuchumi Tanzania.

### Tanzania inapoteza wanyamapori

Licha ya maeneo makubwa yaliyohifadhiwa na mengine yenye wanyamapori yanayochukua karibu asilimia 30 ya eneo la nchi, takwimu za kiutafiti za hivi karibuni zilizoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) mwishoni mwa miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka 2000 na kuchapishwa katika majarida ya kimataifa ya kisayansi zinazonesha wazi kuwa aina, kiasi na mtawanyiko wa wanyamapori Tanzania unaendelea kupungua kwa kasi. **Takwimu hizi bora za kisayansi zinaonesha kupungua kwa wanyamapori katika maeneo yote ya muhimu ya wanyama na mifumo ikolojia yakiwemo maeneo nyeti yaliyohifadhiwa kama vile Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba. Spishi nyingi ukiondoa tu twiga na tembo zimepungua kwa kasi kwa idadi zao tangu katikati ya miaka ya 1980.**

*Kwa kushirikiana na*

*© JMT 2008*

## CHAPISHO NA. 2: SABABU ZA KUPUNGUA

MASUALA MUHIMU:

⇨ Tanzania imeonesha dhamiri imara juu ya uhifadhi wa wanymaapori na bioanuai ikitenga kiasia cha asilimia 30 ya ardhi kama maeneo yaliyohifadhiwa ambako makazi ya binadamu yamezuiliwa.

⇨ Hata hivyo hifadhi hizo na mapori ya akiba mara nyingi hayakidhi haja ya hifadhi ya wanyamapori katika maeneo husika. Spishi nyingi zinahitaji raslimali ambazo zinapatikana nje ya maeneo yaliyohifadhiwa katika misimu fulani kwa mwaka. Pia wanyama wengi wanaishi nje ya maeneo yaliyohifadhiwa wakati wote.

⇨ Uhifadhi hutegemea wanyamapori waliohifadhiwa ndani ya mipaka ya hifadhi na mapori ya akiba na pia nje ya maeneo haya katika ardhi za vijiji na ardhi binafsi.

⇨ Tanzania bado haijafanikiwa vizuri kuhifadhi wanyamapori walio nje ya maeneo yalioyohifadhiwa. Hii ni kwa sababu jamii na watu binafsi hawajaona motisha ya kuhifadhi wanyamapori. Kisheria maduhuli yaliyokusanywa huenda hazina na taasisi za serikali. Kiwango kidogo sana cha maduhuli hubakizwa au hurudishwa kwa jamii au watu binafsi.

⇨ Idara ya Wanyamapori pia ina upungufu wa raslimali unaosabibishwa na mfumo huo wa kugawana mapato.

⇨ Ili wanyamapori wahifadhiwe ni lazima kisheria kuwepo thamani ya kiuchumi kwa jamii ambayo ndiyo yenye maamuzi juu ya matumizi ya raslimali zilizo katika ardhi zao.

⇨ Sekta binafsi na vyama huru ni budu kutoa mchango katika uandaaji wa viwango, matendo ya kiusimamizi na mifano ya biashara bunifu kwa uratibu na Idara ya Wanyamapori.

## KWA WANYAMAPORI TANZANIA

### Kwanini wanyamapori hupungua Tanzania?

Leo hii Tanzania imetenga asilimia 30 ya ardhi yake kama maeneo yaliyohifadhiwa ambako watu wamezuiliwa kuishi. Mataifa machache duniani yameweza kufanya hivyo. Idadi ya Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba yamepanuliwa mfufulizo tangu uhuru. Kwa hiyo, kwa nini wanyamapori hupungua?

### *1. Maeneo yaliyohifadhiwa hayawezi kujitosheleza yenyewe*

Sehemu ya kwanza muhimu ya maelezo ni kwamba katika maeneo mengi duniani hifadhi na mapori ya akiba siku zote havikidhi haja kwa uhifadhi wa wanyamapori katika eneo husika. Sababu ni kwamba maeneo hayo hayajitoshelezi. Wanyamapori huondokea nje ya mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa mara nyingi kwa sababu raslimali kama chakula na maji hupatikana nje ya maeneo hayo. Kama wanyamapori wangeweza kubaki ndani ya mipaka ya hifadhi na mapori ya akiba mathalani kwa kuweka uzio wa kuwazuia wanyama ndani, idadi ingepungua haraka. Hii ni kweli kwa wanyama wanaohama kama vile nyumbu na tembo. Kwa kawaida wanyamapori huhitaji maslahi ya kiikolojia kipindi fulani cha mwaka ambayo hupatikana nje ya mipaka ya hifadhi kama vile nyanda za malisho, maji, maeneo ya kupumzikia na maeneo ya kuzalia.

### *2. Kisheria wanyamapori hawawanufaishi vya kutosha wanajamii*

Wanyamapori wanapotea katika maeneo ya vijiji kwa sababu tatu muhimu:

⇨ Serikali humiliki wanyamapori lakini haina uwezo wa kuwalinda wanyama katika vijiji na ardhi binafsi nje ya maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba.

⇨ Jamii hubeba gharama za kuishi na wanyamapori lakini mara nyingi hawapati manufaa kisheria.

Kama wanyamapori wana gharama zaidi kuliko faida kwa wanavijiji hivyo wanavijiji watafanya kila wawezalo kuwaondoa wanyamapori ili waweze kuboresha maisha yao na ustawi wa familia zao. Kwa mfano watapanua mashamba na kuharibu makazi ya wanyamapori kwa sababu kilimo kina faida na wanyamapori huleta hasara.

⇨ Usimamizi wa sasa wa wanyamapori Tanzania hautoi mifumo yenye tija kwa kuwezesha jamii zifaidike kisheria kutokana na wanyamapori.

## CHAPISHO NA. 3: KUKUZA MADUHULI KUTOKANA NA MATUMIZI ENDELEVU YA WANYAMAPORI

MASUALA MUHIMU:

⇨ Wanyamapori ni moja ya maliasili muhimu Tanzania na chanzo nyeti cha uchumi shindani katika Taifa.

⇨ Ili kupata manufaa makubwa kutokana na wanyamapori ni muhimu kuhimiza soko shindani la uwazi kwa kuwa na uhakika wa kuwatumia wanyamapori kupitia shughuli za utalii wa uwindaji na ule wa picha.

⇨ Tatizo la uwindaji usio na thamani haliwezi kutatuliwa na serikali kwa kupandisha bei za kulipia vitalu vya uwindaji na nyara. Si serikali wala makampuni ya uwindaji anayeelewa bei ingekuwaje. Ni kwa kupitia tu soko shindani la uwazi tunaweza kupata bei halisi.

⇨ Utalii wa picha na ule wa uwindaji ni njia mbadala za kutumia wanyamapori. Uwindaji huleta maduhuli mengi kutoka kwa wageni lakini utalii wa picha unaweza kupanuka na kukua haraka kuliko ule wa uwindaji.

⇨ Uwindaji wa kiutalii utaendelea kuwa ni muhimu hasa katika maeneo yale ambayo yana uwezekano mdogo wa utalii wa picha (utalii wa kuona wanyama) ambako hubakia ndiyo uchaguzi pekee wa kutumia wanyama.

⇨ Katika maeneo ambayo utalii uko juu, kiuchumi inalipa zaidi kwa kuwatumia wanyamapori kwa kupitia utalii wa picha. Uwindaji wa kitalii unaweza kufanyika pamoja na utalii wa picha kama kuna mipango mizuri.

⇨ Idara ya Wanyamapori inahitaji kufadhiliwa vizuri na kupewa raslimali ili kusimamia kwa tija wanyamapori kwa kushirikiana na sekta binafsi, jamii na mashirika ya hiari. Kwa sasa hakuna uwekezaji wa kutosha katika sekta ya wanyamapori nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

### Wanyamapori wanaweza kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi

Idadi ya wanyamapori Tanzania ambayo ni kubwa kuliko nchi yoyote Afrika na duniani inathaminiwa na utalii wa picha na ule wa uwindaji. Kwa hiyo wanyamapori ni chanzo cha uchumi shindani wa Taifa. Hii ina maana kuwa Tanzania ina tabia za asili ambazo zinaifanya kuwa nzuri kuliko nchi nyingine katika kuendeleza wanyamapori na kuiuzia dunia kupitia uwindaji wa kitalii na utalii wa picha. Wakati Tanzania ikiwa na vyanzo muhimu vya maduhuli na biashara kama vile kahawa, maua na korosho, ni rahisi zaidi kwa nchi nyingine duniani kushindana na Tanzania katika biashara ya mazao haya.

Kwa sasa wanyamapori ni moja ya raslimali nyeti Tanzania. Ni thamani kuu katika biashara ya kitalii inayokadiriwa kufikia dola za kimarekani milioni 862 (TZS trilioni 1.03) kwa mwaka 2006. Utalii umekuwa ni moja ya vichocheo vikuu vya ukuaji wa uchumi na urejeshwaji wa uchumi kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita.

Wanyamapori hutoa msingi wa **utalii wa uwindaji Tanzania,** ambayo na ni moja ya maeneo makubwa Afrika katika uwindaji (ya pili tu kutoka Afrika Kusini).

### Taratibu za Mikataba ya Vitalu vya Uwindaji

Ni kanuni ya msingi ya kiuchumi kwamba ushindani wa wazi uwepo kati ya wanunuzi kwa kununua bidhaa kufuatia maamuzi ya soko kwa bei nzuri na sahihi ya bidhaa. Hii ndiyo maana, kwa mfano, wafugaji katika Tanzania hupeleka mifugo yao sokoni kuiuza kwa kila soko la wiki ili waweze kupata bei nzuri ya kuuza bidhaa zao katika soko shindani. Hii inaitwa **sheria ya 'ugavi na mahitaji.'**

**Somo tunalojifunza kutokana na uzoefu huu ni kwamba tatizo la kuweka thamani ndogo ya maeneo ya uwindaji haliwezi kutawaliwa na utaratibu wa kuongeza ada ya maeneo ya uwindaji na nyara za wanyamapori. Si serikali wala makampuni ya uwindaji wanaelewa 'bei sahihi' iweje.**

Ni kupitia tu ushindani wa soko miongoni mwa makampuni kwa maeneo ya uwindaji itahakikisha Tanzania inaweza kukuza mapato kutokana na uwindaji wa wanyamapori. **Ni soko tu linaloelewa bei halisi!** Uwepo uhakiki wa kuwa soko linaendeshwa kwa haki na kwa tija na halijaghushiwa. Kwa kukosekana kwa uwazi na mifumo shindani ya kugawanya maeneo ya uwindaji siku zote kutatoa na kulea mianya ya ufisadi katika ugawanyaji wa vitalu vya uwindaji.

### Kuwianisha uwindaji wa kitalii na utalii wa picha

Uwindaji wa kitalii na utalii wa picha ni njia mbili tofauti lakini zote ni muhimu kiuchumi na kifedha kwa kuzalisha maduhuli na uwekezaji dhidi ya

wanyamapori. Uwindaji wa kitalii huleta ada kubwa kutoka kwa mgeni kuliko utalii wa picha. Hata hivyo, uwindaji unaweza tu kuchukua idadi ndogo ya wateja katika eneo husika kila mwaka kwa sababu wanyama wanaoweza kuwindwa kiutaratibu ni wachache na hivyo kundi moja tu la wateja laweza kuwinda eneo moja kwa wakati moja.

Kiyume chake, utalii wa picha unaweza kupokea wateja wengi na zaidi ya maelfu ya watu wanaweza kuona na kupiga picha simba mmoja ndani ya Serengeti, wakati ni mwindaji mmoja anayeweza kupiga simba katika kitalu cha uwindaji ndani ya Selous. Utalii wa picha una bei ya chini lakini una mauzo makubwa kuliko uwindaji. Tofauti nyingine ni kwamba utalii wa picha huhitaji miundombinu zaidi - kama barabara, makambi, hoteli - wakati uwindaji wa kitalii huweza kufanyika mahala ambapo hakuna miundombinu ya kudumu. Utalii wa picha, kwa sababu huhusisha wageni wengi, huvutia uwekezaji, ajira na mapato kupitia huduma mbalimbali - hizi huitwa '**matokeo zidisho**.'

Tofauti kati ya uwindaji wa kitalii na utalii wa picha kuna viashiria muhimu kwa jitihada za kukuza pato la Taifa kutokana na wanyamapori. Kwa ujumla, uwindaji wa kitalii ni njia muhimu ya kupata mapato kutokana na wanyamapori katika maeneo ya asili yasio na miundombinu, mandhari za kuvutia na idadi kubwa ya wanyamapori ambavyo ni vivutio vya utalii wa picha. **Lakini pale utalii wa picha unapokomaa mapato kutokana na kuongezeka kwa utalii wa picha yanaweza kuzidi mapato yanayozalishwa na uwindaji wa kitalii.**

## Uwekezaji duni katika usimamizi wa wanyamapori

Katika ngazi ya kijamii kumekuwa na urejeshwaji duni wa matumizi ya wanyamapori, mafao na haki za kusimamia na hizo ni sababu muhimu katika kupungua kwa idadi ya wanyamapori na hiyo inaweza kuonekana pia kama ni uwekezaji duni.

Takwimu za serikali zinaonesha kuwa TANAPA ina uwezo wa kutumia takribani dola za kimarekani 1,130 kwa kila kilomita ya mraba kwa mwaka kwa ajili ya usimamizi wa wanyamapori, wakati Idara ya Wanyamapori inaweza tu kutumia kiasi kinachofikia dola za kimarekani 24 katika kilomita moja ya mraba kwa mwaka.

Hata hivyo, mwaka 2007 Hifadhi za Taifa (TANAPA) walipata TShs bilioni 69.0 lakini ni asilimia 1.8 tu zilipelekwa kwa shughuli za ujirani mwema (TANAPA Annual General Report 2007). Kinyume chake, katika mwaka 2006 Idara ya Wanyamapori ilipata TShs bilioni 15.3 kutokana na matumizi endelevu ya wanyamapori, na ilikuwa na uwezo wa kurudisha asilimia 12.8 katika wilaya husika (Economic Survey 2006).
Kwa nini ni mapato kidogo sana hurudishwa kwa jamii na usimamizi wa wanyamapori - hususan kwa TANAPA - wakati wanyama wanaendelea kupungua?

Ni wajibu wa serikali kuwekeza katika wanyamapori kama raslimali ya umma. Kulingana na umuhimu wake kiuchumi haishauriwi kuendelea 'kumkamua ng'ombe hadi akauke.' Hii ni kuiomba Idara ya Wanyamapori, Serikali za Mitaa, Asasi zilizoidhinishwa na Jamii kukifikia kisichowezekana.

*Mchoro wa dhana kuonesha jinsi muundo wa mapato kutoka sekta ya wanyamapori ungepaswa kuwa. Hazina hukusanya tu kodi za ongezeko la thamani, zingine zinawekezwa katika usimamizi wa wanyamapori na maendeleo ya jamii.*



## CHAPISHO NA. 4: USIMAMIZI WA WANYAMAPORI NA KUPUNGUZA UMASKINI

MASUALA MUHIMU:

⇨ Wanyamapori wangeweza kutoa mchango mkubwa kisheria katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa jamii zinazoishi katika maeneo yenye wanyamapori.

⇨ Kwa sasa wanyamapori wana thamani katika jamii zinazofaidika na biashara haramu ya wanyamapori.

⇨ Maendeleo katika kuendeleza usimamizi wa kijamii wa wanyamapori kupitia maeneo ya hifadhi za jamii umekuwa wa utaratibu na aghali.

⇨ Haki kamili za kusimamia na kufaidika kutokana na wanyamapori zinahitaji kurudishwa katika ngazi ya jamii mapema iwezekanavyo ili kutoa motisha chanya juu ya usimamizi endelevu wa wanyamapori miongoni mwa vijiji vinavyopatika kando ya wanyamapori.

⇨ Kama wanyamapori hawataonesha nafasi katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa jamii, hivyo shughuli zingine za kiuchumi zitachukua nafasi, na wanyama wataendelea kupungua na kutoweka. Na hii ni kwa sababu wananchi hawatakuwa na utetezi wa kiuchumi ili kuwasimamia wanyamapori kwa njia endelevu.

## Nafasi ya wanyamapori katika kupunguza umaskini

Ni muhimu kuhakikisha kuwa wanyamapori wanatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania (angalisa Chapisho Na. 3). Ni muhimu pia kuwa wanyamapori watoe mchango mkubwa katika kupunguza umaskini na kukuza utajiri katika ngazi ya kijamii. Umuhimu wa kuboresha uhusiano kati ya uchumi wa kitaifa na kupunguza umaskini ngazi ya jamii ndiyo mada kuu katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). MKUKUTA unaahidi jitihada za kuhakikisha kuwa mafao ya ukuaji uchumi yanasambaa hadi vijijini kwa wanajamii na maskini.

***Kikwazo kikuu katika kufikia fursa hii ni kwamba tangu wakati wa ukoloni jamii zilizuiliwa kisheria kutumia wanyamapori na haki za kutumia wanyamapori zilibakia na kuthibitiwa na serikali.***

## Maeneo ya Hifadhi za Jamii (WMA)

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ilielekeza mabadiliko ya kisheria yatakayoruhusu uundwaji wa WMA mahali ambapo jamii wangekuwa wasimamizi kisheria na kufaidika na wanyamapori katika ardhi za vijiji.

Katika mwaka 2002 serikali iliunda kanuni za kuongoza WMA, zilizorejewa mwaka 2005, chini ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974 ambayo inaruhusu uanzishwaji wa maeneo ya hifadhi za jamii katika ardhi za vijiji. Kuanzia Januari 2003 Waziri wa Maliasili ya Utalii amefanya kazi na jamii, Serikali za Wilaya na mashirika binafsi mbalimbali ili kuanzisha maeneo ya hifadhi za jamii yapatayo 16 kwa nchi nzima. Hadi Septemba 2008 maeneo kumi ya hayo yalitangazwa kama WMA, na baadhi ya hayo yalikuwa yameshaingia katika mikataba ya uwekezaji.

Wakati jitihadi zimefanyika katika kuanzisha WMA, matatizo ya kimsingi yamekwamisha maendeleo:

⇨ Awali, kanuni za uanzishwaji maeneo ya WMA ziko changamano na jamii zinahitaji msaada kutoka nje ili kutimiza masharti yote. Hii imehafifisha uanzishwaji wa WMA. Maeneo hayo kama yalivyoanzishwa ni aghali sana kuyaendeleza.

⇨ Pili, maeneo ya WMA hayatoi mamlaka ya kutosha kuthibiti mafao ya kiuchumi kwa jamii kutokana na wanyamapori.

## Kufikiria aina mbadala juu ya usimamizi wa wanyamapori kijamii

Zaidi ya WMA kuna njia zingine ambazo jamii zinaweza kupata manufaa ya kiuchumi kutokana na wanyamapori. WMA zimeanzishwa kutoa haki kwa jamii juu ya matumizi ya wanyamapori lakini pia utalii usio wa uvunaji waweza kufanyika katika ardhi za vijiji ambako WMA hazijaanzishwa, kwa vile utalii wa kupiga picha hauvuni wanyamapori.

Kaskazini mwa Tanzania, vijiji vimeingia katika mikataba na wawekezaji ili kuendesha utalii ambao utaleta faida kwa jamii kutokana na wanyamapori. Mingi ya mikatabi hii vijiji na wawekezaji iko katika vijiji kuzunguka hifadhi za Serengeti and Tarangire, na imekuwepo zaida ya miaka 10 hadi 15 iliyopita. Kumekuwepo na mawakala mbalimbali wa serikali ambao wamesaidia kusukuma jitihada hizo.

## CHAPISHO NA. 5: MASLAHI YA JAMII: UMUHIMU WA KUSHIRIKISHA SEKTA MBALIMBALI

MASUALA MUHIMU:

- ⇨ Ili kuweza kukuza mchango chanya wa wanyamapori kwa maslahi ya jamii na shughuli za kiuchumi, ni muhimu kuchukua mtazamo wa kushirikisha sekta tofauti ili kuratibu usimamizi wa wanyamapori pamoja na sekta za ardhi, utalii, misitu na mifugo.
- ⇨ Matendo ya usimamizi wa wanyamapori huweza kuleta migogoro na vijiji vyenye hati za ardhi hasa kupitia mwingiliano wa Mapori Tengefu na Ardhi za Vijiji.
- ⇨ Usimamizi wa wanyamapori na hifadhi ya misitu ya jamii katika ngazi ya kijiji vinahitaji kuwianishwa ili kutoa manufaa ya kutosha vijijini, kwa sababu wanyamapori na misitu ni raslimali zinazoweza kupatikana kwa pamoja katika ardhi za pamoja za vijiji.
- ⇨ Matendo na sera ya usimamizi wa wanyamapori vinatakiwa kuwianishwa na malengo ya ukuaji wa sekta ya utalii kitaifa, ili kuwanufaisha wananchi.
- ⇨ Usimamizi wa wanyamapori ni budi uwe na uwiano wa sera ya sekta ya mifugo pamoja na malengo ya maendeleo kwa vile wanyamapori na mifugo vyote vinategemea nyanda za malisho na vyanzo vya maji katika maeneo mengi na husabibisha ushindani na wakulima.
- ⇨ Mtazamo wa kuhusisha sera nyingi ni muhimu ili kuweka thamani kubwa kwa wanajamii waweze kufaidika kutokana na ardhi na raslimali zilizopo.

### Nafasi ya wanyama katika kupunguzu umaskini

Usimamizi ulioboreshwa wa wanyamapori ungeweza kutoa manufaa mengi kwa jamii. Lakini pia ingeweza kusimamiwa kusaidia mahitaji ya jamii katika njia ambayo ni pana zaidi. Kile ambacho kingeleta maana zaidi kwa jamii ni kuwa na ‘maeneo ya <u>usimamizi maliasili kijamii</u>’ ambako vyote raslimali, wanyamapori na misitu vinasimamiwa katika ngazi ya kijiji badala ya kutenganishwa kama maeneo ya WMA na misitu ya vijiji. Kupitia mazingira wezeshi ya kisera hii ingekuwa rahisi katika maeneo mengi ambayo yana vyote, WMA na misitu ya vijiji.

## CHAPISHO NA. 6: DESTURI NZURI KATIKA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI KUJIFUNZA KUTOKA KATIKA KANDA

MASUALA MUHIMU:

- ⇨ Pote mashariki na kusini mwa Afrika wanyampori ni raslimali muhimu , lakini nchi zingine zimekuwa na desturi zenye usimamizi wenye tija kuliko nchi zingine.
- ⇨ Nchini Kenya, wanyama wamepungua kwa asilimia 50 tangu katikati ya miaka ya 1970, kwa sababu katazo la uwindaji wa mwaka 1977 inapunguza chaguzi za kiuchumi kwa serikali, jamii na watu binafsi kutokana na wanyamapori. Ambako biashara imara za utalii wa picha zina msingi mzuri na kuzalisha mapato kwa wenye ardhi, wanyamapori Kenya wameongezeka au kuendelea sawa mathalani Kajiado na Laikipia.
- ⇨ Namibia inayo mmoja ya mifumo yenye mafanikio mazuri ya usimamizi wa wanyamapori katika Afrika, ambako wanyamapori wanaongezeka, thamani ya wanyamapori kitaifa inaendelea kukua, na mapato zaidi ya jamii yanatokana na wanyamapori. Umuhimu wa mfumo wa Namibia ni kwamba wanajamii na wenye ardhi binafsi wana mamlaka ya kufaidika na asilimia 100 ya mapato ya wanyamapori katika ardhi zao.
- ⇨ Somo la msingi kutoka kwa uzoefu na usimamizi wa wanyamapori wa kanda ni kwamba nchi zilizowezesha watu binafsi wa jamii na umoja wa wenye ardhi ili kufaidika na thamani kiuchumi ya wanyamapori, zinaweza kukuza idadi ya wanyamapori na kuongeza mapato kijamii na kitaifa kutokana na wanyamapori.

### Kuendeleza mafanikio na kujumuisha uzoefu wa kanda

Nchi zingine katika kanda zina uzoefu na somo saidizi kwa Tanzania kuhusiana na desturi bora na njia bunifu za kukuza mapato ya matumizi ya wanyamapori - kiuchumi, kiikolojia na kijamii. Kwa ujumla, nchi kusini mwa Afika kama vile Namibia, Botswana, Zimbabwe, na Afrika Kusini zina uwezo wa kusimamia wanyamapori ili idadi ya wanyama wa spishi nyingi imekuwa sawa au kukua, na mafao kutokana na wanyamapori katika ngazi za jamii na Taifa yameongezeka sana. Mashariki mwa Afrika sera na desturi za wanyamapori zina mafanikio machache zaidi.

## CHAPISHO NA. 7: MAPENDEKEZO YA KISERA ILI KUENDELEZA WANYAMAPORI WA TANZANIA

***Wanyamapori huipatia Tanzania soko lenye ushindani katika ulimwengu wa leo wenye utanda wazi ambapo hakuna raslimali nyingine inaweza kutoa.*** Wanyamapori ni raslimali endelevu. Ikiwa Tanzania itaandaa sera na matendo yenye usimamizi endelevu wa wanyamapori, shughuli za kiuchumi zinazotokana na wanyamapori zitaendelea kukua na kupanuka kwa miongo mingi ijayo. Cha kusikitisha ni kwamba wanyamapori wa Tanzania wanapotea, na hivyo kupoteza ushindani katika soko la kikanda kama vile Namibia au Botwana ambako wana idadi ya wanyama inayoongezeka ama iliyotulia, na ambako pia kuna utalii wenye nguvu unaokua hasa ule wa uwindaji na wa upigaji picha.

Kipindi cha miaka ya 1990 Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania ilifanya tathmini ambayo ilihitimisha kwamba:

> ***"Ni muhimu kwa uhifadhi wa wanyamapori hapo baadaye kwa hapa Tanzania wananchi waishio pamoja na wanyamapori wapatiwe mafao ya moja kwa moja yatokanayo na wanyama."***

Ili kuchangia katika jitihada za watunga sera, wadau wote wa kiserikali na wale wasiowa kiserikali na ili wanyamapori wawe na faida kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho, mapendekezo yafuatayo ya kisera yamewekwa na inafaa yasomwe kwa kina katika Chapisho Na 7.

1. KUREKEBISHA SHERIA NA SERA YA WANYAMAPORI ILI KUKABILI CHANGAMOTO ZA SASA NA KUUNDA MFUMO WA KITAASISI KWA AJILI YA USIMAMIZI ENDELEVU WA WANYAMAPORI TANZANIA

2. KUBORESHA NA KUFAFANUA KANUNI ZA UANZISHWAJI MAENEO YA HIFADHI ZA JAMII (WMA) KATIKA ARDHI ZA VIJIJI

3. KUSAIDIA NJIA MBADALA ZA KUWANUFAISHA WANANCHI KUTOKANA NA WANYAMAPORI KUPITIA UTALII WA BIASHARA-UBIA ZA JAMII NA SEKTA BINAFSI

4. KUKUZA THAMANI YA UCHUMI WA WANYAMAPORI KWA KUANZISHA MFUMO WA USHINDANI KATIKA UGAWAJI WA VITALU VYA UWINDAJI KAMA VILE ILIVYO KATIKA ZABUNI AU MINADA YA WAZI

5. SERIKALI IONGEZE MAPATO YA HAZINA KUU KUTOKANA NA WANYAMAPORI IKITILIA MKAZO UKUSANYAJI WA MAPATO YA UPILI – HASA KODI ZILIZOPO, NA KUHAKIKISHA JAMII NA WAMILIKI WA ARDHI BINAFSI WAKIPATA MAPATO YA MOJA KWA MOJA KAMA VILE ADA ZA MAENEO YA UWINDAJI NA UTALII WA PICHA6. KUTATUA MIGOGORO BAINA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI NA HAKI ZA ARDHI YA JAMII

**Kisanduku Na. 1: Mambo muhimu katika kuboresha biashara ya uwindaji wa kitalii**

Kuboresha biashara ya uwindaji wa kitalii ili iweze kuakisi thamani halisi ya soko la wanyamapori katika Tanzania itahitaji maandalizi muhimu kwa upande wa serikali kwa kushirikiana na wawindaji, wataalam na mashirika ya hiari. Imependekezwa na watalaam kwamba **mfumo wa zabuni za wazi ikiwa maombi na viwango** yaweza kuwa ndiyo njia nzuri. Katika kubuni mfumo huo masuala yafuatayo yanahitaji kufikiriwa kwa uangalifu kwa maana ya namna ya kuyafikia yafuatayo:

- Kuyavutia makampuni yenye rekodi nzuri ya usimamizi na utendaji;
- Kuanzisha mfumo wa uwindaji wenye uwiano wa utendaji wa kiuchumi na ulinzi wa raslimali kwa kipindi sahihi na ushindani katika kuomba upya;
- Kujenga **ubia** wa muda mrefu **unaochochewa na utendaji** kati ya serikali na sekta binafsi ikiwa na **ufuatiliaji wa uwazi na tathmini kulingana na vigezo vilivyowekwa**;
- Kutoa vivutio vyenye nguvu kwa ulinzi wa wanyamapori na makazi na kuboresha maeneo ya wanyamapori yaliyoharibiwa ama kupungua kwa thamani ya nyara;
- Kuvutia maslahi katika vitalu vizuri vya uwindaji na vitalu visivyo na mvuto vinavyohitaji kuboreshwa;
- Kuwarekebisha wazabuni wakubwa ambao hawana rekodi nzuri ya kiusimamizi na matumizi ya vitalu vya uwindaji;
- Kuhimiza makampuni ya kitanzania ili yaweze kuingia na kushindana na makampuni ya kutoka nje;
- Kuiyapa makampuni uhuru ili kufikia utendaji wa juu.